

Mgonjwa wa kifua kikuu sugu anaweza kufanya yafuatayo ili kuzuia kuenea kwa maambukizi ya vimelea vya Kifua Kikuu sugu (MDR TB):

- Kukamilisha matibabu ya kifua kikuu sugu kama anavyoelekezwa na mtaalam wa afya
- Kutoacha kutumia dawa kwa sababu zozote zile bila kushauriana na wataalamu wa afya
- Mgonjwa anayetaka kusafiri awasiliane na mtoa huduma wa kifua kikuu sugu ili apatiwe kibali, ushauri wa afya na dawa za kutosha kwa mda wote akiwa safarini na ikibidi apewe rufaa
- Aepuke misongamano
- Kuishi kwenye nyumba yenye mzunguko wa hewa ya kutosha na atumie mda mwingi kukaa sehemu zenye mzunguko mkubwa wa hewa safi kama vile sehemu za nje barazani.



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto



**KUMBUKA:
kifua kikuu sugu kinatibika
bila malipo**

Kwa maelezo zaidi wasiliana na
mtoa huduma wa / za Afya aliye karibu nawe.

Kimetolewa na:

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wazee na Watoto

kupitia

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua
Kikuu na Ukoma

S.L.P. 9083, Dar es Salaam, Tanzania.

Barua pepe: info@moh.go.tz,

Tovuti: www.ntlp.go.tz,

Toleo la 2016

MAMBO ANAYOPASWA KUFAHAMU MGONJWA WA KIFUA KIKUU SUGU



TUUNGANE KUTOKOMEZA KIFUA KIKUU

KIFUA KIKUU SUGU NI NINI?

Kifua kikuu sugu ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea vya kifua kikuu ambavyo vimepata usugu kwa dawa angalau mbili za daraja la kwanza za kutibu kifua kikuu cha kawaida ambazo ni Rifampicin na Isoniazid. Hizi dawa hutumika kutibu watu wote waliougua kifua kikuu cha kawaida (TB)

Aina hii ya ugonjwa wa TB matibabu yake ni ya mda mrefu, na gharama zake ni kubwa

Pia aina hii ni hatari kwa watu wanaoishi na VVU au wenye VVU na wale ambao kinga zao za mwili zimeshuka kutokana na maradhi kama vile saratani, kisukari, utapiamlo, ulevi wa kupindukia n.k. kwani mara tu wapatapo vimelea hivi huugua haraka ugonjwa wa kifua kikuu na wapo kwenye hatari ya kupoteza maisha.

KIFUA KIKUU SUGU KINAENEZWAJE?

Kifua kikuu sugu huenezwa kwa njia ya hewa kama ilivyo kwa kifua kikuu cha kawaida pale mgonjwa anapokohoa au kupiga chafya. Mtu akivuta hewa yenye vimelea wa kifua kikuu sugu ataambukizwa vimelea hivyo. Hivyo basi, ni muhimu pale mgonjwa wa kifua kikuu sugu anapokohoa au kupiga chafya afunike mdomo na pua kwa kitambaa au karatasi laini.

Kifua Kikuu sugu hakienezwi kwa njia ya:

- Kushikana mikono na mgonjwa
- Kula chakula pamoja
- Kushika nguo za kulala au kutumia choo pamoja

DALILI ZA KIFUA KIKUU SUGU

- Kukohoa kwa muda mrefu
- Homa za mara kwa mara
- Kutokwa na jasho jingi kuliko kawaida hasa nyakati za usiku
- Makohozi yenye damu
- Kupungua uzito au kukonda

KIFUA KIKUU SUGU KINASABABISHWA NA NINI?

- Mgonjwa anayeamwa kifua kikuu cha kawaida asipomeza dawa kikamilifu kama alivyoelekezwa na wataalamu wa afya
- Usimamizi duni wa mgonjwa anayekunywa dawa za kifua kikuu. Usimamizi huu unapaswa kufanywa na mhudumu wa afya au msimamizi wa matibabu nyumbani

NANI YUKO KWENYE HATARI YA KUPATA KIFUA KIKUU SUGU?

Watu ambao wapo kwenye mazingira hatarishi ya kupata kifua kikuu sugu (MDR TB) ni:

- Wale wasiotumia dawa za TB kama ilivyoelekezwa na wataalamu wa afya
- Wale wanaougua kifua kikuu kwa mara ya pili baada ya kutumia dawa hizo ndani ya miaka miwili iliyopita
- Wale wanaotoka katika mazingira ambayo ugonjwa wa kifua kikuu sugu upo kwa watu wengi sana
- Wale ambao wametumia muda mwingi kukaa na mgonjwa wa kifua kikuu sugu ambaye hajaanza matibabu, kwa mafano kuishi nyumba moja na mgonjwa huyo

VIWIMO NA MATIBABU YA KIFUA KIKUU SUGU

Mara mgonjwa anapogunduliwa na vimelea vya kifua kikuu sugu kwa njia ya maabara, atianza matibabu ambayo ni tofauti na matibabu ya kifua kikuu cha kawaida. Kifua kikuu cha kawaida hutibiwa miezi sita hadi nane kutegemea na aina ya kifua kikuu wakati matibabu ya kifua kikuu sugu huchukua muda wa miezi kumi na nane (18) mpaka miezi ishirini na nne (24)

kutokana na maendeleo ya mgonjwa wakati wa matibabu.



Kwa sasa matibabu kifua kikuu sugu yanatolewa katika hospitali ya Taifa ya Kifua Kikuu ya Kibong'oto iliyopo mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Siha ambapo mgonjwa anatibiwa kwa miezi 6-8 mpaka anapokuwa hawezi kuambukiza jamii halafu anaruhusiwa kuendelea na matibabu hospitali/ kituo cha afya au zahanati iliyo karibu na nyumbani kwake. Serikali hugharimia matibabu ya kifua kikuu sugu ambayo hutolewa bila malipo kwa mgonjwa.

